


**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 8, Issue 1, 2025**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Balagha Katika Hotuba za Wagombea Wawili wa Urais Kwenye Makongamano ya Wajumbe Nchini Kenya, Mwaka wa 2022

*Bi. Caroline Kathure Kamuru[1*], Dkt. John Khaisie Wanyama, PhD[1] na Dkt. Timothy Kinoti M'Ngaruthi PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu Cha Embu, S. L. P. 6-60100, Embu, Kenya.
[*] ORCID ID; https://orcid.org/0009-0008-2074-9269; Barua pepe ya mawasiliano: kathure.caroline@embuni.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*30 Juni 2025*

**Istilahi Muhimu**:

*Balagha, Mantiki, Maadili, Kigusahisi, Hotuba, Makongamano, Wajumbe na Wagombea wa Urais.*

**IKISIRI**

Balagha ni mkakati ambao hutumika katika mawasiliano ili kushawishi hadhira lengwa. Utafiti huu ulilenga kuchanganua matumizi ya balagha katika hotuba za wagombea wawili wa urais, wakati wa makongamano yao ya kitaifa ya wajumbe nchini Kenya, mwaka wa 2022. Wagombea hao walikuwa William Samoei Ruto na Raila Odinga. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Balagha ya Aristotle. Nadharia hii, ilisaidia mtafiti katika kutambua matumizi ya balagha, maadili, kigusahisi na mantiki kama yalivyothibitika katika hotuba nne zilizowasilishwa. Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka kwa rekodi rasmi za hotuba hizo kutoka kwa mtandao wa YouTube. Mtafiti alitumia mbinu ya kimakusudi kuangazia matumizi ya balagha katika hotuba zilizotolewa na wagombea wawili wakuu wa urais. Hii ni kutokana na uzoefu wao wa muda mrefu katika siasa na nafasi yao ya kipekee katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2022. Data ilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo kwa kufuata mihimili ya nadharia ya balagha. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha matumizi ya aina tatu kuu za balagha ambazo ni; mantiki, kigusahisi na maadili. Utafiti uligundua kuwa balagha ilitumika hasa kujenga imani, kugusa hisia, kuonyesha uwezo wa uongozi, na kueleza sera zao. Kazi hii inatarajiwa kuwa na mchango muhimu kwa usomi katika uwanja wa lugha na mawasiliano, mawasiliano ya kisiasa na kusaidia wanajamii kupata maarifa ya kuwawezesha kung'amua ghiliba za wagombea. Utafiti ulihitimisha kuwa balagha ina jukumu muhimu katika mawasiliano ya kisiasa na ushawishi wa wapiga kura. Hata hivyo, balagha inafaa itumike kwa ujuzi na si kwa lengo la kuidanganya hadhira lengwa bali kwa kutumia urazini na maadili katika azma ya wagombea.

**APA CITATION**

Kamuru, C. K., Wanyama, J. K. & M'Ngaruthi, T. K. (2025). Balagha Katika Hotuba za Wagombea Wawili wa Urais Kwenye Makongamano ya Wajumbe Nchini Kenya, Mwaka wa 2022. *East African Journal of Swahili Studies*, *8*(1), 490-504. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

**CHICAGO CITATION**

Kamuru, Caroline Kathure, John Khaisie Wanyama and Timothy Kinoti M'Ngaruthi. 2025. "Balagha Katika Hotuba za Wagombea Wawili wa Urais Kwenye Makongamano ya Wajumbe Nchini Kenya, Mwaka wa 2022". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (1), 490-504. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

**HARVARD CITATION**

Kamuru, C. K., Wanyama, J. K. & M'Ngaruthi, T. K. (2025) "Balagha Katika Hotuba za Wagombea Wawili wa Urais Kwenye Makongamano ya Wajumbe Nchini Kenya, Mwaka wa 2022", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(1), pp. 490-504. doi: 10.37284/jammk.8.1.3230

**IEEE CITATION**

C. K., Kamuru, J. K., Wanyama & T. K., M'Ngaruthi "Balagha Katika Hotuba za Wagombea Wawili wa Urais Kwenye Makongamano ya Wajumbe Nchini Kenya, Mwaka wa 2022", *EAJSS*, vol. 8, no. 1, pp. 490-504, Jun. 2025.

**MLA CITATION**

Kamuru, Caroline Kathure, John Khaisie Wanyama & Timothy Kinoti M'Ngaruthi. "Balagha Katika Hotuba za Wagombea Wawili wa Urais Kwenye Makongamano ya Wajumbe Nchini Kenya, Mwaka wa 2022". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 1, Jun. 2025, pp. 490-504, doi:10.37284/jammk.8.1.3230.

## UTANGULIZI

Uchaguzi wa urais wa 2022 nchini Kenya uliashiria wakati muhimu katika siasa zake. Hotuba zilizotolewa na wagombea urais wakati wa makongamano ya wajumbe ziliwapa nafasi muhimu ya kuunda maoni ya umma na kupata uungwaji mkono. Lugha ni chanzo cha kujipa na kudhihirisha mamlaka (Nurkhamidah na wengine, 2021). Katika neni za kisiasa, lugha hutumika kuanzisha, kujenga na kuimarisha uhusiano miongoni mwa wawasilianaji (Al-Aadili, 2024).

Wanenaji hutumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano. Balagha ni mkakati ambao hutumika kusababisha ushawishi (Grimaldi, 2020). Wagombea walio na ujuzi wa balagha huitumia kwa njia ya ufanifu ili kufikisha ujumbe wao kwa hadhira lengwa. Wagombea wa urais huteua lugha yao kwa uangalifu ili kuendana na yale yatakayowasaidia kupendelewa zaidi dhidi ya wapinzani wao. Kulingana na (Nyako, 2013) shughuli za kisiasa hudhihirishwa kupitia hotuba zinazotolewa na wagombea kwa hadhira lengwa. Kupitia hotuba, wanasiasa huwashawishi na kudhibiti jinsi hadhira itakavyopokea na kuelewa ujumbe unaowasilishwa. Kusudi kuu la ujumbe wa kisiasa ni kuhalalisha msimamo wa kisiasa unaoaminika kuwa bora zaidi. Ili kufanikisha hili, wanasiasa huwasilisha jumbe zao kwa umakini na kwa njia ambayo inaweza kukubalika kwa urahisi na hadhira.

Mawasiliano yenye mafanikio huhitaji uelewano kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Matamshi yanapowasilishwa, maana fulani hukusudiwa. Msikilizaji hutarajiwa kuwa na uwezo wa kufasiri vyema maneno yanayosemwa na mzungumzaji ili kuelewa vyema maana na lengo lililokusudiwa. Walakini, mazungumzo mengi huwa hayafanikishwi baina ya mnenaji na mskilizaji. Hii ni kwa sababu wasikilizaji wengi huwa hawaelewi au kufasiri lengo kuu lililokusudiwa na mzungumzaji, (Haucsa na wengine, 2020). Hadhira lengwa mara nyingi hupumbazwa na wanasiasa wanapotumia maneno yaliyojaa balagha kwa kuwaghilibu na kuwashawishi wanapolenga kuungwa mkono. Jambo hili hutokana na mkatiko wa mawasiliano unaotokea baina ya mgombea na hadhira lengwa (Kamuhabwa, 2021). Jinsi sentensi zao huundwa ili kufikia hadhira kubwa huonyesha matumizi ya balagha (Habwe, 1999). Kupitia hali hii ya kughilibiwa na kuzuzuliwa kwa hadhira lengwa, mara nyingi huchangia uteuzi wa viongozi wasio bora. Kwa sababu hii, utafiti huu ulidhamiria kuchunguza mikakati mbalimbali ya balagha katika hotuba za wagombea wakuu wa kiti cha urais nchini Kenya.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

## MAPITIO YA MAANDISHI

Katika uchaguzi wa Marekani wa mwaka wa 2020, wagombea wa urais walitumia balagha katika hotuba zao. Joe Biden aliyeibuka mshindi alitumia mikakati mitatu ya balagha katika mazungumzo yake. Kigusahisi katika mazungumzo yake kilitumika kwa kiwango cha juu zaidi (Nurkhamidah na wengine, 2021). Tafiti hizi mbili zinahusiana kwani zinaongozwa na nadharia ya balagha kama ilivyoelezwa na Aristotle. Utafiti wake una mchango katika kuangazia vipengele muhimu vya nadharia ya balagha katika diskosi ya kisiasa. Tofauti na utafiti wa Nurkhamidah aliyeangazia hotuba ya rais aliye mamlakani, utafiti huu uliangazia matumizi ya balagha katika hotuba za wagombea wawili wa urais wakati wa mikutano yao ya wajumbe, nchini Kenya kabla ya kupata mamlaka.

Kwa kuangazia matangazo ya magazeti, utafiti ulifanywa kuchunguza balagha nchini Ghana ili kuleta athari ya ushawishi kwa wasomaji (Torto, 2020) . Aligundua kuwa, lugha huwezesha hadhira kutambua bidhaa na kuikumbuka kwa urahisi. Utafiti huu unahusiana na wa Torto kwani unaongozwa na nadharia ya Aristotle ya balagha. Hata hivyo, utafiti wa Torto unatofautiana na huu kwani ulilenga vipengele vya ushawishi vinavyotumiwa katika matangazo ya magazeti nchini Ghana ilhali utafiti huu unaangazia vipengele vya ushawishi vya balagha katika hotuba za wagombea wa urais. Tafiti zote mbili zinachangiana na kuoana vyema kwani zote zinaangazia matumizi ya balagha katika lugha ili kuleta ushawishi kwa hadhira husika.

## Misingi ya Nadharia

Utafiti uliongozwa na nadharia ya Aristotle ya balagha (1954). Aristotle anafafanua vithibitisho vitatu vya kisanii vinavyounda sanaa ya balagha kuwa pamoja na mantiki, kigusahisi na maadili (Kamuhabwa, 2021).

### *Mantiki*

Mantiki ni neno la Kiingereza linalotokana na neno la Kigiriki '*logos*' lenye maana ya mawazo yenye kuungwa mkono na matendo yenye maana na ithibati (Torto, 2020). Uthibitisho sahihi huweza kutumika kudhihirisha hoja zenye mantiki. Ushahidi hujitokeza pale ambapo pana mawazo yenye mkusanyiko wa ukweli halisi na data kitakwimu. Mantiki ina maana ya kushawishi kwa matumizi ya hoja zenye kudhihirisha maarifa ya mambo, ujuzi wa uchanganuzi, uwezo wa kukumbuka mambo kwa urahisi na matumizi ya maneno yenye ithibati. Ni vyema mnenaji kuwasilisha mawazo na hoja zake kwa kifupi na inavyoeleweka. Ili kunata zaidi umakini wa hadhira lengwa, ni vyema kuzingatia mpangilio unaofaa katika maongezi (Madon na wengine, 2021). Zifuatazo ni sifa za mantiki;

- Matumizi ya lugha rahisi inayoeleweka na hadhira lengwa
- Uthibitishaji wa maarifa ya mnenaji
- Matumizi ya sitiari
- Matumizi ya lugha chanya na hasi

### *Kigusahisi*

Kigusahisi hulenga kuchochea hisia za hadhira lengwa kwa kuihusisha katika miktadha mbalimbali. Hisia za binadamu hufanikisha na kuathiri mikondo ya ufikiriaji. Ni vichochezi vyenye nguvu ambavyo huumua mioyo na akili za watu binafsi kukubaliana na madai ya mzungumzaji (Grimaldi, 2020). Kigusahisi hulenga kugusa moyo na hisia za mnenewa ili ashawishike na kufungua roho yake, akubali yanayosemwa na mnenaji bila kuuliza maswali, ajihusishe na mnenaji kifikra na akubaliane naye kimsimamo. Mihemko (hisia) ikitawala, nyoyo hulegea; nyoyo zikilegea akili hutekwa nyara. Wanasiasa hutumia udhaifu huu kuwaelekeza wapiga kura katika hali ya kuwaamini kipumbavu na hata kuwasujudu.

Sifa za kigusahisi;

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

- Matumizi ya lugha ya kuzua mihemko
- Lugha ya kuzua matumaini ili kuchochea hisia
- Masimulizi ya kibinafsi na tajriba alizopitia mnenaji.
- Ulinganisho wa kiistiari
- Masimulizi ya habari yenye uwezo wa kusisimua hisia na kuchochea hadhira kuchukua hatua fulani.

***Maadili***

Ni uaminifu ambao mzungumzaji huweka na hadhira kutokana na utu na tabia yake. Hadhira lengwa huwajibika kumpa mnenaji mamlaka kutokana na maadili aliyonayo. Ni imani ambayo mnenaji huweka kwa hadhira na hujenga uhusiano mkuu kati yao wakati wa mazungumzo (Higgins & Walker, 2012). Busara na uaminifu wa mzungumzaji kwa hadhira hupatikana kupitia utu wake, tabia zake, namna anavyojiwasilisha mbele ya hadhira, upevu wa akili zake ikiwemo ujuzi wa masuala ibuka katika jamii, nia njema, uadilifu na usikivu (Qotrunnada, 2020).

Sifa za maadili;

- Uadilifu na uwajibikaji wa mnenaji
- Uelewa wa kina wa mambo
- Masimulizi ya kudhihirisha uaminifu na heshima
- Matumizi ya historia na utaalamu
- Kujenga uaminifu na uadilifu wa mnenaji

Maadili hudhihirika kupitia umuhimu mnenaji anaipa hadhira na anavyoaminika na hadhira lengwa. Mtumiaji wa mkakati huu hulenga kufaidika kutokana na thamani na itikadi za wanajamii. Mara nyingi, jambo hili hugusia masuala kama; uzalendo, utamaduni, haki na demokrasia, dini, jinsia na thamani za kifalsafa.

Katika muktadha wa kisiasa wa Kenya, wanasiasa wamevutiwa na mikakati ya matumizi ya lugha kiufundi na balagha katika harakati zao za kushawishi wapiga kura. Maelezo haya yanathibitisha wazo la Aristotle kwamba balagha lazima iambatane na mahitaji ya hadhira, na hivyo kuthibitisha umuhimu na uhalali wa nadharia ya Aristotle ya balagha katika uchanganuzi wa hotuba za wagombea urais nchini Kenya, mwaka wa 2022 (Karanja, 2022).

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa kithamano. Kulingana na Neuman (2003), kama ilivyonukuliwa katika (Gerstlé & Nai, 2019), mbinu ya kithamano ni njia bora zaidi ya kufahamu maana fiche kwa kuunganisha habari tofauti na kubadilisha mitazamo. Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumika ili kupata data ya kukidhi kusudi la kubainisha aina za balagha. Mtafiti alikusanya data yake kutoka kwa hotuba nne zilizorekodiwa kwenye kanda za video za makongamano hayo manne. Data hii ilichukuliwa kutoka kwa mtandao wa YouTube.

Data ya utafiti ilikuwa maneno, virai, sentensi, vifungu, aya ama kauli zilizotolewa na wagombea wa urais. Mtafiti alicheza kanda za video na rekodi za makongamano ya wagombea wawili wa urais wa mwaka wa 2022 mara kadhaa huku akisikiliza kwa makini ili aweze kufikia lengo la utafiti. Data iliyokusanywa ilisimbwa ili iweze kufasiriwa. Mtafiti alichanganua data kwa misingi ya mihimili ya nadharia ya Aristotle. Mtafiti alitumia ule ujuzi na maarifa alio nao kutathmini na kufasiri data kisha akaeleza matokeo ya utafiti kimpangilio.

## UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

Katika uchanganuzi wa hotuba za wagombea wawili wa urais wa Kenya, ilibainika kuwa mihimili yote mitatu ya balagha ilitumika katika hotuba. Mihimili yenyewe ni: mantiki, kigusahisi na maadili.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

**Mantiki**

Mantiki ni ushawishi unaotegemea hoja zenye uthibitisho. Kulingana na Torto (2020), hoja zenye data thabiti huimarisha ushawishi kwa hadhira lengwa. Uwepo wa mantiki hudhihirishwa na matumizi ya lugha rahisi, maarifa ya mnenaji, matumizi ya sitiari, uwepo wa ithibati na matumizi ya lugha chanya na hasi. Aidha, hudhihirishwa na matumizi ya lugha yanayoeleweka na hadhira, masimulizi ya kibinafsi na ulinganishaji wa mambo. Mantiki huboresha ushahidi na hivyo kuimarisha madai ya mnenaji. Wagombea wote wawili walidhihirisha data thabiti katika hotuba zao za kisiasa ifuatavyo:

***Matumizi ya Lugha Rahisi inayoeleweka na Hadhira***

Dhana hii ilidhihirishwa na kauli zifuatazo:

William Ruto alisema: "UDA ndicho chama cha kila '*hustler*' nchini Kenya. Hiki ndicho chama ambacho hautaulizwa kuhusu jina la baba yako, akaunti yako ya benki. Hiki ndicho chama cha kila Mkenya kutoka kila nyanja ya maisha. Ninajivunia sana kama Mkenya leo, kwa sababu mmenipa jukumu la kuwa kiongozi wa chama hiki kikubwa." **WR1**

Mzungumzaji alitumia hoja zilizojenga dhana ya uhusishaji wa chama cha UDA na wananchi wote kwa jumla. Mnenaji alilenga kuishawishi hadhira kukubaliana naye kwamba chama hicho hakibagui. Hii ni mbinu ya kuwasilisha hoja kwa kutumia dhana zinazoeleweka kwa urahisi na jamii. Kulingana na nadharia hii, mnenaji alipotumia lugha inayoeleweka kwa urahisi na hadhira, alilenga kuishawishi na kujenga uelewano wa haraka pia baina yao. Neno "*hustler*" hutumiwa na watu wengi katika jamii hasa ya kisasa, hivyo kueleweka kwa urahisi na watu wengi. Aliposema kuwa, chama cha UDA ni cha kila "*hustler*" alilenga uhusiano wa karibu baina yake na hadhira lengwa. Hoja hii, ililenga kuwashawishi wamuunge mkono. Mnenaji alitumia neno "*hustler*" kimaksudi kwa kuwa hujumuisha walio wengi katika jamii.

Raila Odinga alisema;

Naahidi kuwa kazi katika ofisi za umma zitaongozwa na nidhamu, uchapakazi, ufanisi, uwepo wa ari ya juu na maadili. Hakutakuwa na upendeleo, ukabila au ufisadi wa aina yoyote. Hivyo, ukitia bidii utaweza kufanikiwa kadri na uwezo wako. **RO1**

Mnenaji alitumia dhana ya uongozi bora ili kuonyesha utawala aliopendekeza kwa kujenga hoja za usawa, haki na demokrasia. Kwa kufanya hivyo, alijenga hoja yenye ushawishi kwa kuwa inawiana na matarajio ya hadhira kuhusu utawala bora. Kauli yake inaonyesha matumizi ya mantiki katika kujenga taswira ya uongozi wake. Hivyo, kauli hii ilihitimisha wazo la jumla kwamba uongozi wake ungewasaidia wengi bila upendeleo. Ikiwa kuna usawa katika uongozi, maendeleo hupatikana kwa wengi. Jambo hili lilizua dhana ya ushawishi kwa hadhira kwani lina matumizi ya fikra madhubuti yanayoendana na matumaini yao. Hoja hii ilikuwa na uwezo wa kushawishi hadhira lengwa kwa kuwa iliguzia baadhi ya mambo yanayofahamika na kukubalika katika jamii. Katika mataifa ambayo hakuna ubaguzi, huwa na ustawi wa kifedha na kuwezesha maendeleo katika sekta mbalimbali.

***Maarifa ya Mnenaji***

Raila Odinga alionyesha dhamira yake ya kuboresha uchumi wa nchi ya Kenya kwa kusema:

"Ninaahidi kutumia teknolojia katika kila shamba nchini Kenya na kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo; Wakulima watasaidika katika kuzalisha zaidi kutokana na jasho la kazi yao kwa kutumia mbolea ya bei nafuu." **RO2**

Mgombea alionyesha ana maarifa kuhusiana na mambo tofauti yanayoikumba jamii. Aliposema hivi, alirahisisha uwezo wa hadhira kumwamini kwani alionyesha kuwa ana uelewa wa mambo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

wanayoyapitia katika maisha yao ya kila siku. Alitumia hoja za kimantiki kama vile *"teknolojia"* na *"mapinduzi"* kudhihirisha namna ambavyo angetatua changamoto zinazodhihirika katika kilimo. Kimantiki, ni matamanio ya kila mkulima kupata mazao bora. Mara nyingi, hili huwa haliwezekani hasa kwa wale wakulima wadogo kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali za kutosha. Hata zikiwepo, huwa za bei ghali, hivyo inakuwa vigumu kwa kila mkulima kufaidika. Aliahidi kuboresha sekta hii kupitia teknolojia na mbolea ya bei nafuu. Hoja hii ililenga kuwashawishi wakulima kwa kuwa iliendana na matarajio yao. Alilenga hadhira imwamini na iamini alichokisema kwa kuwa, ukulima ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi ya Kenya. Matokeo haya yanalingana na utafiti wa (Madon na wengine, 2021) ambao ulieleza kuwa mnenaji anaweza kuishawishi hadhira kwa matumizi ya hoja zenye kudhihirisha utambuzi wa mambo na kutumia maneno yenye ithibati.

### *Matumizi ya Sitiari*

Raila Odinga alisisitiza umuhimu wa umoja nchini Kenya katika uchaguzi kwa kusema;

"Umoja, umoja, umoja. Kuwaleta Wakenya pamoja ni vita ambavyo tunapaswa kupigania na tushinde. Ni ombi langu kwamba Wakenya wote wataungana kulipigania hili kwa kuwa linastahili." **RO3**

Kauli hii ilitumia sitiari ya "vita" kuashiria kuwa umoja haupatikani kwa urahisi bali unahitaji juhudi. Hivyo, kauli hii ilichochea hisia za uzalendo kwa hadhira, jambo ambalo watu wengi huenzi. Maneno kama *"tunapaswa kupigania na tushinde"* yalijenga matumaini kwamba umoja si ndoto bali jambo linaloweza kufikiwa iwapo watu watajitolea. Sitiari ya vita mara nyingi hutumiwa katika muktadha wa mapambano dhidi ya jambo, hivyo kuhamasisha watu kuwa na imani ya hatma njema. Lugha yake pia iliashiria wajibu wa pamoja, hivyo kuhamasisha uhusishaji wa kitaifa. Mzungumzaji, alitumia mantiki iliyofanikishwa na matumizi ya lugha ya msisitizo na sitiari.

### *Matumizi ya Lugha Chanya na Hasi*

William Ruto anaeleza namna ambavyo angepambana na ufisadi mahakamani kwa kusema;

"Siku ya kwanza nikiingia ofisini, nitaidhinisha bajeti ya mahakama ili kuweka mahakama huru. Mahakama inafaa ipewe fedha za kushughulikia kazi zao ikiwemo kutekeleza jukumu lao la kutatua migogoro, kuhakikisha wahalifu wanawekwa rumande na wafisadi wanapata nafasi yao katika jela. Kuhakikisha kuwa wana uhuru katika kutekeleza majukumu yao bila vikwazo vinavyowapata kupitia kutopewa fedha za kuendeleza shughuli zao… Tunaamini katika uhuru wa mahakama… Tunataka mahakama ambayo kwa hakika ni huru. Ambayo haipokei simu kutoka kwa viongozi wakuu wa serikali ili kuhukumu." **WR2**

Mzungumzaji alitumia lugha chanya na hasi kwa mpangilio wa kimkakati ili kuwasilisha msimamo wake kuhusu uhuru wa mahakama na vita dhidi ya ufisadi. Kwa kutumia lugha chanya, alijenga taswira ya matumaini na mabadiliko chanya kwa kusisitiza umuhimu wa kuiwezesha mahakama kifedha ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aliposema *"nitaidhinisha bajeti ya mahakama ili kuweka mahakama huru,"* alitumia lugha chanya kujidhihirisha kama mleta suluhu kwa kuiwezesha mahakama kifedha. Hata hivyo, alitumia lugha hasi kuonyesha changamoto zilizopo, kama mahakama kuathiriwa na ukosefu wa fedha na ushawishi wa viongozi wakuu wa serikali. Kauli yake, *"Mahakama ambayo haipokei simu kutoka kwa viongozi wakuu wa serikali,"* iliashiria udhaifu wa mfumo uliopo. Mbinu hii ililenga kushawishi hadhira kwa kuwaonyesha nia thabiti ya kufanya mabadiliko aliyopendekeza kuwa ya muhimu na ya dharura.

Kwingineko, alipendekeza, uboreshwaji wa idara mbalimbali kama inavyodhihirishwa na mfano ufuatao:

"Wametumia Tume ya Maadili ya Kupambana na Ufisadi, idara ya upelelezi na makosa ya jinai na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

Shirika la Ukusanyaji wa Ushuru kuendeleza harakati za kisiasa. Tutaboresha taaluma ya ofisi ya Maadili ya Kupambana na Ufisadi na Shirika la Ukusanyaji wa Ushuru ili waweze kutekeleza wajibu wao kisheria na kikatiba. Siku ya kwanza, tutateua afisa wa fedha kwa ajili ya Inspekta Jenerali (IG) na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai (DCI) ili baadaye, DCI na IG wawe na uhuru wa kifedha na wasitegemee tena Ofisi ya Rais kuendeleza majukumu yao. Kama walivyotumia vibaya KRA tutafanya kinyume kabisa. Tutaboresha taaluma ya KRA, tutatumia mfumo wa kidijitali kwa KRA, na kuhakikisha inakusanya kodi zote kitaalamu. Asilimia 60 ya kodi ambazo hazikusanywi kama VAT, tutahakikisha tunaunda mifumo na majukwaa ya kidijitali ili tuweze kukusanya kodi hizo bila kupigana na biashara za Wakenya au kuziharibu." **WR3**

Mzungumzaji alitumia lugha hasi kukosoa matumizi ya taasisi kama EACC, DCI, na KRA kwa malengo ya kisiasa badala ya kutekeleza majukumu yao ya kisheria. Aliposema, *"Wametumia… kuendeleza harakati za kisiasa"* ilijenga picha ya ufisadi uliohitaji kutatuliwa. Jambo hili lilionyesha udhaifu wa mfumo uliopo. Katika upande wa lugha chanya, Ruto alijenga tumaini la kutoa suluhisho. Aliahidi, *"Tutaboresha taaluma ya EACC na KRA"* na *"Tutatumia mfumo wa kidijitali kwa KRA"* ili kuongeza uwazi na ufanisi wa ukusanyaji wa kodi. Alihamasisha imani katika utawala wake kwa kusisitiza uwazi na ufanisi wa kiteknolojia badala ya ukandamizaji wa biashara. Pia, alisisitiza uhuru wa kifedha kwa DCI na IG ili kuepuka utegemezi kwa Ofisi ya Rais. Kwa ujumla, alitumia lugha hasi kudhoofisha mfumo uliokuwepo na kuonyesha kasoro zake, huku lugha chanya ikitumika kuwasilisha mabadiliko aliyokusudia kama suluhisho la kuimarisha taasisi za kupambana na ufisadi na ukusanyaji wa ushuru. Hii ilimsaidia kujenga taswira ya kiongozi anayeleta mageuzi kwa njia thabiti na ya haki.

**Kigusahisi**

Kigusahisi ni mbinu ya kushawishi kwa kugusa hisia za hadhira. Huchangia uwezekano wa hadhira lengwa kuelewa mtazamo wa mnenaji, kukubali hoja zake na kuchukua hatua fulani kulingana na maombi yake. Kulingana na utafiti, wagombea walitumia kigusahisi ifuatavyo:

***Matumizi ya Lugha ya Kuzua Mihemko***

Katika muktadha wa siasa, mbinu hii hutumika kwa ufanisi mkubwa ili kuleta umoja, kuhamasisha uungwaji mkono, au hata kufifisha ukosoaji. Kauli ifuatayo inadhihirisha mbinu hii.

"Kama Naibu Rais, nimefanya kazi moja kwa moja na wananchi kwa kuwaendea vijijini mwao, masokoni, mashambani, na maeneo yao ya kazi, nikiwa na lengo la kutekeleza uongozi wa kusikiliza zaidi na kuzungumza kidogo. Katika safari yangu ya kisiasa, daima nimeamini katika kushirikiana na wananchi, kuwasikiliza, na kufanya kila niwezalo kutimiza matakwa yao, badala ya kujenga kumbukumbu ya mafanikio yangu binafsi. Nimejifunza kuwa ofisi zetu za kifahari, tulivu, na salama hazifikiki kwa wengi wanaozihitaji zaidi. Kama kiongozi, huu ni udhaifu mkubwa kwa sababu unatusababisha kupoteza fursa ya kuwa wa msaada na wenye ufanisi." **WR5**

Kauli hii inatumia lugha ya kuzua mihemko kwa kujenga uhusiano wa karibu na wananchi, kugusa hisia za mshikamano, na kuonyesha unyenyekevu wa mnenaji. Kwa kusema *"nimefanya kazi moja kwa moja na wananchi"* na *"kuwafikia vijijini mwao, masokoni, mashambani, na maeneo yao ya kazi"*, anajionyesha kama kiongozi anayewasiliana moja kwa moja na wananchi wa kawaida. Hivyo, kuwafanya wahisi kuwa anaelewa changamoto zao. Aidha, kauli kama *"kusikiliza zaidi na kuzungumza kidogo"* zinawasilisha picha ya kiongozi mnyenyekevu anayejali maoni ya wananchi badala ya kutumia mamlaka yake kuamua kwa niaba yao. Hii inachochea hisia za imani na matumaini, huku

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

akijitofautisha na viongozi wanaoonekana kuwa mbali na wananchi.

Zaidi ya hayo, mnenaji anatumia lugha ya kuonyesha dosari kwa kusema *“ofisi zetu za kifahari, tulivu, na salama hazifikiki kwa wengi wanaozihitaji zaidi”*, akisisitiza pengo kati ya viongozi na wananchi wa kawaida. Hii inazua hisia za kusikitisha na kutia msukumo wa mabadiliko. Kwa kueleza kuwa huu ni *“udhaifu mkubwa”*, msemaji anazua hali ya haraka kwa wasikilizaji, akiwafanya waone kuwa kuna haja ya uongozi mpya unaojali zaidi wananchi. Lugha hii inawafanya wananchi wajihisi kuwa sehemu ya safari ya kisiasa ya mnenaji, lakini pia inaweza kutafsiriwa kama mbinu ya kisiasa ya kujionyesha kuwa mkombozi bila kutoa suluhisho mahususi.

William Ruto pia anatoa kauli hii:

“Kwa njia ya kipekee nawashukuru viongozi wengi, maseneta, magavana na wabunge waliodhihirisha ujasiri na kujitolea kuunganisha chama ambacho kina zaidi ya wanachama milioni saba.” **WR6**

Mgombea urais William Ruto, alitumia maneno kama “kwa njia ya kipekee”, “ujasiri”, “kujitolea” kusisitiza hisia za shukrani na heshima kubwa kwa viongozi waliounga mkono chama cha UDA. Aliwapa viongozi hadhi maalum kwa kuonyesha juhudi zao katika kuunganisha chama, jambo lililowafanya wahisi kuthaminiwa na kuheshimiwa. Kwa njia hii, anawahamasisha kujiona kuwa sehemu ya mafanikio makubwa na hivyo kuendeleza mshikamano wao na chama. Alipotaja “wanachama milioni saba”, anasisitiza ukubwa wa mafanikio, jambo linaloweza kuamsha hisia za mshikamano na fahari miongoni mwa wanachama hicho.

### *Lugha ya Kuzua Matumaini ili Kuchochea Hisia*

Katika hotuba za kisiasa, matumizi ya taarifa zinazobeba ujumbe wa matumaini, mshikamano, na maendeleo mara nyingi hutumika kama mkakati wa kuhamasisha hadhira kuchukua hatua fulani. Matamshi ya kisiasa yenye lugha yenye mvuto huchochea hisia za matumaini kwa mustakabali bora, huku yakihimiza mshikamano wa jamii na uwajibikaji wa pamoja. Moja ya mbinu zinazotumiwa ni kusisitiza uwezekano wa ndoto na matarajio kutimia, jambo linaloweza kuwafanya wananchi wahisi kuwa wao ni sehemu ya mchakato wa maendeleo.

William Ruto alisema:

Kenya inaweza kuwa mahali ambapo ndoto za kila raia zinatimia kupitia juhudi za pamoja na mazingira mazuri ya kiuchumi. **WR8**

Alipotumia maneno kama *"ndoto za kila raia zinatimia"* alidhamiria kuwapa watu matumaini na kuwafanya waamini kuwa wangeweza kufanikisha malengo yao ikiwa mazingira yangeboreshwa. Kauli hii ilisisitiza “juhudi za pamoja” ikihimiza mshikamano na uwajibikaji wa kila mmoja katika kujenga taifa bora. Pia ilitoa wito wa kuchukua hatua aliposema, “mazingira mazuri ya kiuchumi”. Jambo hili lingewafanya watu waone kuwa kuna haja ya kushiriki katika kujenga uchumi imara ili kutimiza ndoto zao. Kauli ililenga kuhamasisha raia kushirikiana ili kufanikisha ndoto zao kupitia juhudi za pamoja na maendeleo ya kiuchumi.

Raila Odinga alisema:

Umoja, Umoja, Umoja. Kuunganisha Kenya ni vita tunavyopaswa kupigania na kushinda. Ni maombi yangu kwamba Wakenya wote watajiunga na juhudi hizi. Ni dhamira yenye thamani… Hili linatokea leo. **RO4**

Hapa, mnenaji aliishawishi hadhira kwa kutumia lugha ya kuchochea hisia za matumaini na uwajibikaji wa pamoja. Aliporudia neno “umoja” mara tatu, alilenga kusisitiza umuhimu wa kushirikiana. Matumizi ya maneno kama *“vita tunavyopaswa kupigana na kushinda”* yaliunda taswira ya dhamira ya pamoja na uharaka wa hatua. Aidha, mnenaji alitumia lugha ya kujenga imani kwa hadhira kwa kueleza kuwa uongozi wenye

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

maono na ujasiri unaweza kuleta maendeleo ya kweli, akihamasisha wananchi kuungana katika juhudi za sasa *"hili linatokea leo"*.

### *Lugha ya Shukrani kama Mbinu ya Kuimarisha Uaminifu wa Kisiasa*

Raila Odinga alitumia lugha ya shukrani kama mbinu ya kushawishi hadhira yake alipokubali uteuzi wake kama mgombea wa urais wa chama cha Azimio la Umoja mwaka 2022. Alisema:

"Hii ni mojawapo ya nyakati ambazo unahisi unakosa maneno ya kuelezea shukrani zako. Ningependa kuanza kwa kutoa shukrani zangu kwa nyote ambao mmefika hapa leo na kufanya uamuzi wa kuniteua kama mgombea wenu katika uchaguzi ujao. Ningependa kusema kwamba nakubali uteuzi wa Azimio la umoja kugombea urais wa jamhuri ya Kenya katika uchaguzi mkuu wa Agosti 2022. Nakubali uteuzi huu kwa shukrani kubwa na kwa kujitolea kwa watu wote, nchi yetu, na viongozi wote pamoja na vyama vilivyopitisha uteuzi huu." **RO5**

Katika kauli hii, msemaji alitumia kigusahisi kwa kuonyesha hisia za unyenyekevu na shukrani kwa wafuasi wake. Alipotamka kuwa ni vigumu kupata maneno ya kuelezea shukrani zake, alilenga kujenga hisia za umoja na hadhira, akiwafanya wahisi kuwa sehemu muhimu ya mchakato wa kihistoria. Mbinu hii inawafanya wafuasi wake kujihisi kuthaminiwa, jambo linaloweza kuongeza uaminifu na mshikamano wao kisiasa.

Aidha, alipoeleza kuwa anakubali uteuzi *"kwa shukrani kubwa na kwa kujitolea kwa watu wote"*, alijitambulisha kama kiongozi anayewakilisha maslahi ya wote, si kundi fulani pekee. Hili lilikuwa na lengo la kuimarisha uungwaji mkono wake kwa kuonyesha kwamba anajali ustawi wa kila Mkenya. Kutambua mchango wa kila mmoja katika mchakato wa uteuzi ni njia ya kuonyesha unyenyekevu, ambayo huongeza uhusiano wa karibu kati ya kiongozi na wafuasi wake.

Kwa mujibu wa (Nyako, 2013), lugha ya shukrani ina nguvu ya kujenga mshikamano na kuongeza uaminifu wa kisiasa. Katika muktadha wa hotuba hii, Raila Odinga alitumia shukrani si kama kauli ya kawaida tu, bali kama chombo cha kushawishi wapiga kura waendelee kumuunga mkono kwa kura au kushiriki katika kampeni zake. Hii inathibitisha kuwa shukrani katika siasa si tu tendo la heshima bali pia ni mbinu madhubuti ya kushawishi na kujenga uhusiano thabiti wa kisiasa.

### *Lugha ya Umoja kama nyenzo ya Kisiasa*

Raila Odinga, alieleza dhana ya umoja wa kitaifa kupitia kauli;

Azimio ni chama pana cha kitaifa cha kidemokrasia inayoweka kipaumbele katika masuala ya umoja wa kitaifa, maendeleo jumuishi na matumizi ya rasilimali za umma kwa uwazi na uwajibikaji. Tutakitumia kuendeleza vita dhidi ya umaskini, ujinga na bado ni kazi inayohitaji kukamilishwa. **RO6**

Kauli hizi zinatumia mbinu ya ufafanuzi wa kisera ili kueleza maono na malengo ya chama cha Azimio la Umoja. Kwa kuieleza Azimio kama *"chama pana cha kitaifa cha kidemokrasia"*, msemaji alijenga picha ya chama kinachowakilisha maslahi ya taifa nzima badala ya kundi fulani. Alipozungumzia *"umoja wa kitaifa, maendeleo jumuishi na matumizi ya rasilimali za umma kwa uwazi na uwajibikaji"*, alitumia lugha inayoonyesha dhamira ya chama kushughulikia masuala ya utawala bora na ushirikishwaji wa wananchi wote. Zaidi ya hayo, kwa kutaja *"vita dhidi ya umaskini na ujinga"*, msemaji aliangazia changamoto za kijamii na maendeleo ambazo chama chake kilikusudia kushughulikia. Msemaji alisisitiza kwamba umoja si jambo la kufikirika kwa vizazi vijavyo bali ni hali inayojengeka kwa wakati huu. Hii ililenga kuhamasisha na kuleta matumaini kwa hadhira lengwa. Matumizi ya "sisi" na "tunafanya" yaliimarisha hisia za uwajibikaji wa pamoja.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

William Ruto alieleza dhana ya msingi ya kuunganisha taifa kupitia kauli:

Tuwe daima tukijitahidi kuishi kulingana na misingi yetu ya kuunganisha taifa letu kupitia jitihada jumuishi na shirikishi za kutafuta nafasi kwa kila mtu. **WR9**

Kauli hii ina nguvu kwa sababu inalenga mshikamano wa kitaifa, ambao ni nguzo muhimu ya utawala bora. Kwa kusisitiza *"jitihada jumuishi na shirikishi,"* mgombea anajenga picha ya uongozi unaowapa watu wote nafasi sawa bila ubaguzi. Hisia za haki na usawa ni zana muhimu katika siasa, kwani huwafanya wananchi kuhisi kuwa wanajumuishwa katika mfumo wa kiutawala. Katika muktadha wa uchaguzi, hotuba za aina hii huwa zenye mvuto kwa wapiga kura, kwani zinatoa matumaini na maono ya pamoja ya maendeleo. Kauli hii inahusiana na kigusahisi katika nadharia ya Aristotle, kwa sababu inagusa hisia na kuleta dhana ya umoja.

***Masimulizi ya Kibinafsi na Tajriba za Mnenaji***

William Ruto alitumia masimulizi ya kibinafsi ili kuimarisha uhalisia wa hotuba yake na kujenga uhusiano wa karibu na hadhira. Anatoa mawazo yake akiwa naibu rais kwa kusema:

“Agano letu liliunda msingi wa mtazamo mpya wa siasa zenye misingi ya masuala mahususi, ambazo ziliwekwa rasmi kupitia vyama vya kisiasa vya kitaifa. Tulifanikiwa kuonyesha kwamba demokrasia haiambatani na matukio hasi au hali ya kutokuwa thabiti. Tumeonyesha kwamba demokrasia haijidhihirishi kupitia ubaguzi, kutengwa, mgawanyiko, mashaka au migogoro. Katika serikali, tulijikita katika kutekeleza miradi na mipango iliyowezesha serikali kuwafikia wananchi mahali walipo na kulingana na mahitaji yao. Kwa hivyo, tulibadilisha nchi kwa haraka kupitia uwekezaji katika miundombinu, kama msingi wa utoaji huduma bora, ufanisi na maendeleo katika sehemu zote za Kenya.” **WR10**

Maneno haya yalitumia masimulizi ya kibinafsi na tajriba za mnenaji ili kuimarisha hoja zake kuhusu demokrasia na maendeleo ya taifa. Kwa kutumia maneno kama *"tulifanikiwa kuonyesha," "tumeonyesha,"* na *"tulibadilisha nchi,"* mnenaji anajihusisha moja kwa moja na mabadiliko aliyoyasimamia, akijipa uhalali wa kushuhudia na kueleza mafanikio hayo. Alijenga uaminifu kwa hadhira yake kwa kusisitiza kuwa alipokuwa naibu rais, serikali yao ilitekeleza miradi kwa ufanisi, ikiwemo uwekezaji mkubwa katika miundombinu kama msingi wa utoaji huduma bora. Kauli yake kwamba *"Agano letu liliunda msingi wa mtazamo mpya wa siasa zenye misingi ya masuala mahususi"* ilionyesha tajriba yake katika uundaji wa sera, huku akieleza kuwa uongozi wake ulikuwa wa utulivu na wa maendeleo badala ya mgawanyiko. Kwa kutumia masimulizi ya kibinafsi, mnenaji alijitambulisha kama sehemu ya historia ya kisiasa ya taifa na alihimiza hadhira yake kutambua mchango wake katika kubadilisha nchi kwa haraka kupitia sera na utekelezaji thabiti wa miradi.

William Ruto alitoa Kauli hii pia:

Nimejifunza kuwa kosa kubwa ambalo serikali au chama kinaweza kufanya ni kushindwa kupita mtihani wa kuleta umoja. Fikra zangu za awali za kisiasa ni kwamba uongozi unahusu watu na maendeleo yanaweza kuwa endelevu tu ikiwa mipango itatengenezwa kwa misingi ya mahitaji na matarajio ya watu. **WR11**

Wanasiasa hutumia mbinu hii ili kuonyesha kuwa wanaelewa changamoto za jamii kwa undani, na hivyo kuonekana kuwa sehemu ya watu wanaowaongoza. Mnenaji alitumia mtazamo wa kibinafsi alipotumia kauli ya “Nimejifunza…” ikionyesha uzoefu wa moja kwa moja wake alipotafakari kuhusu siasa na uongozi. Hadhira inaweza kushawishika kwa kuamini kuwa mnenaji ana uelewa wa kina kuhusu siasa na amejifunza kutokana na makosa au changamoto za awali. Kauli hii ilieleza hitimisho ambalo mnenaji alifikia baada ya kutathmini uongozi wa serikali na vyama vya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

kisiasa. Alijifunza umuhimu wa umoja na maendeleo yanayozingatia mahitaji ya watu. Hivyo, kauli hii inaonyesha mtazamo wa mnenaji kuhusu siasa na uongozi kupitia uzoefu wake binafsi. Katika usemi wa kisiasa, mvuto kama huu ni wenye ufanisi kwa kuimarisha imani na mshikamano, kwani huwafanya hadhira lengwa kuhisi kuthaminiwa na kuhamasishwa kuunga mkono mtazamo au sera za mnenaji. Hivyo, ingawa matumizi ya hadithi za kibinafsi yanaweza kuwa na manufaa katika kuongeza uhalisia wa hotuba za kisiasa na kujenga imani kati ya mnenaji na hadhira, ni muhimu kwa hadhira kuwa na umakini katika kuchambua ukweli wa simulizi hizo.

***Ulinganisho wa Kiistiari***

Wanasiasa hutumia mbinu hii ili kuwasilisha ujumbe mzito kwa njia isiyo wazi. William Ruto alitoa kauli hii kudhihirisha hili.

Muundo mpya wa umoja wa kitaifa wa vijana ulitungwa kwa njia zisizo za kidemokrasia na kwa masharti yaliyohalalisha kumalizwa kabisa kwa upinzani na uvunjaji wa katiba ili kuafiki mipangilio ya kikabila iliyojaa ufisadi na hatari. Wakati huo huo, ajenda kuu ya *Big Four* ilitupiliwa mbali na kusukumwa nyuma, huku utekelezaji wa miradi yake muhimu ukiachwa mikononi mwa nguvu za kutekwa kwa serikali na maslahi binafsi. Wale waliobaki waaminifu kwa maono yetu ya awali walitengwa, wakafutiliwa, wakatishiwa na hatimaye kuteswa. Hivi ndivyo tulivyopoteza miaka minne ambayo ingetupeleka kwenye ustawi mzuri wa ndoto iliyojaa matumaini na iliyowahamasisha mamilioni ya Wakenya mnamo 2013. **WR12**

Matumizi ya kigusahisi katika kauli hii inaonekana kupitia lugha ya kiistiari, ambapo mgombea analinganisha ndoto nzuri ya 2013 na hali halisi ya miaka minne ya baadaye iliyojaa mateso na kupoteza matumaini. Hisia za huzuni na masikitiko zinajitokeza kwa kutumia maneno kama *"kuangamizwa kwa upinzani"* na *"uvunjaji wa katiba"*, kuashiria usaliti wa kisiasa. Aidha, anasisitiza jinsi waliobaki waaminifu kwa maono yao walivyotengwa, kufutiliwa mbali, kutishiwa na hatimaye kuteswa, jambo linalochochea huruma kwa waliokumbwa na hasira kwa wale waliotekeleza haya. Ulinganisho wa kiistiari unajidhihirisha katika kauli *"tulipoteza miaka minne ambayo ingetupeleka kwenye ustawi mzuri wa ndoto"* ambapo neno "ndoto" lilitumika kiistiari. Liliwakilisha haki za kiuchumi na kijamii za Wakenya ambazo zingepatikana kwa kubuni ajira kwa mamilioni ya vijana, kubadilisha sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji na kuboresha uchumi, na kwa kutekeleza mpango wa huduma za afya kwa wote. Matumizi ya sitiari yalihakikisha kwamba ujumbe wake uliolenga kudhihirisha umuhimu wa *Big Four* agenda umepitishwa kwa njia ya ufasaha, na kugusa wasikilizaji kwa hisia za huzuni, hasira na huruma, hivyo kuongeza ushawishi wake.

Akifananisha changamoto za taifa na safari ya meli, Raila Odinga alisema:

"Hakuna abiria anayepaswa kuachwa nyuma katika meli hii." **RO8**

Kauli hii ilitumia taswira na ulinganisho wa kiistiari. Ilifananisha maendeleo ya taifa na *safari ya meli*. Neno "meli" limetumika kiistiari kuwakilisha nchi na neno "abiria" linawakilisha Wakenya. Kimsingi, meli huendeshwa na nahodha mmoja mkuu huku akishikwa mkono na wasaidizi wake. Ulinganisho huu ulijenga picha yenye nguvu inayotafsiri maendeleo kama harakati za pamoja zinazohitaji mshikamano na ushirikishwaji wa kila mtu. Kwa kutumia taswira ya *abiria wasioachwa nyuma*, ilisisitiza usawa wa kijamii na dhamira ya kuhakikisha kila Mkenya angehusika na kufaidika na maendeleo ya taifa. Hii ni mbinu yenye nguvu ya kisiasa kwa sababu inahamasisha umoja na inaifanya hadhira lengwa kuhisi kuwa wana wajibu wa kushiriki katika maendeleo ya taifa lao. Matumizi haya ya kigusahisi yalilenga kuvutia hisia za wapiga kura, kuhamasisha mshikamano, na kujenga imani kwa wagombea.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

**Maadili**

Maadili hujidhihirisha kwa sifa zifuatazo; Uaminifu na heshima, uadilifu na uwajibikaji, uelewa wa kina wa mambo, uwajibikaji na uwazi, sifa ya historia na utaalam, dhana ya uadilifu na uaminifu. Matumizi ya maadili yalibainika kama ifuatavyo:

***Uadilifu na Uwajibikaji wa Mnenaji***

Katika hotuba yake, William Ruto alijitokeza kama kiongozi mwenye rekodi ya uwajibikaji na nidhamu kazini aliposema:

Nimetekeleza majukumu yangu kwa uaminifu na hakuna hata kazi moja ambayo rais alinipa ambayo sikuitimiza kikamilifu. **WR13**

Mzungumzaji alilenga kuivutia hadhira yake kwa kudhihirisha uaminifu wake katika kutekeleza majukumu aliyopewa na kuimarisha imani ya wapiga kura kwake. Kwa kusema *"kwa uaminifu,"* anasisitiza kuwa utendaji wake umejengwa juu ya misingi thabiti ya maadili. Aidha, anapotamka kwamba hakuna hata kazi moja ambayo rais alinipa ambayo sikuitimiza kikamilifu, anajenga taswira ya mtu wa kutegemewa. Hii inaendana na mtazamo wa Aristotle kwamba maadili hujengwa kupitia tabia njema, busara na rekodi ya utendaji wake wa awali. Ruto analenga kuonyesha kuwa ana tabia ya uwajibikaji na kwamba hadhira yake inapaswa kumwamini kwa sababu ya rekodi yake ya utendaji. Hata hivyo je, hadhira ina ushahidi wa kuthibitisha madai yake? Je, kuna wanaohoji uaminifu wake? Katika muktadha wa kisiasa, upinzani mara nyingi huhoji ikiwa wagombea kweli wamekuwa waaminifu na wenye uwajibikaji au wanatumia maneno tu kama njia ya kujinufaisha kisiasa. Pia alithibitisha utekelezaji wa majukumu kwa ufasaha akisema kazi zote alizopewa alizitimiza kikamilifu. Kauli hii inajikita katika uaminifu na uwajibikaji anaposema “kwa uaminifu”. Inasisitiza maadili ya kazi ambayo yanaweza kupimwa na kuthibitishwa kupitia historia ya utendaji wake.

***Uelewa wa Kina wa Mambo***

Raila Odinga alionyesha uelewa wa kina wa mambo katika kujenga hoja zake za kisiasa aliposema:

Ninaahidi kuongoza mapambano dhidi ya umaskini, ukosefu wa ajira, na hali ya kukosa msaada nchini Kenya. Na kutekeleza Kipengele cha 43 cha Katiba yetu, ambacho kinawahakikishia Wakenya haki ya kupata elimu, afya, chakula, maji, makazi, na usalama. Hakuna Mkenya hata mmoja anayepaswa kuhisi kusahaulika katika nchi yetu. **RO9**

Anaporejelea katiba, anafanya hoja yake ionekane kuwa si tu ahadi za kisiasa bali wajibu wa kikatiba. Inaongeza uzito wa mazungumzo yake kwa kutoangazia muktadha wa kibinafsi na kujiweka kama mtetezi wa haki za wananchi kwa kuongozwa na katiba. Kwa mujibu wa Aristotle, maadili haiwezi kujengwa kwa maneno matupu pekee inahitaji uhalali na mamlaka halisi kama uelewa wa katiba. Katika nadharia ya Aristotle, maadili huimarishwa zaidi pale mzungumzaji anapodhihirisha uelewa wa kina wa mazingira ya hadhira yake. Kwa kujihusisha na matatizo yao moja kwa moja, anajenga picha ya uongozi unaowajibikia watu wote. Kwa mujibu wa (Habwe, 2016) maadili ya kiongozi huimarika pale anapojitambulisha kama mtu mwenye uzoefu, uadilifu, na uaminifu. Odinga alitumia hoja za kikatiba kuonyesha uadilifu wake, alijikita kwenye matatizo ya wananchi kuonyesha uaminifu wake, na alijitambulisha kama suluhisho la changamoto za kijamii, hivyo akijenga picha ya uzoefu wake. Ingawa kurejelea Katiba kunaongeza uhalisia kwa hoja yake, hadhira bado inahitaji kuona mikakati thabiti ya utekelezaji ili kuthibitisha dhamira yake.

***Uaminifu na heshima***

William Ruto anatoa kauli hii kudhihirisha hili:

"Tunahitaji upinzani si kwa ajili ya kuleta mfarakano, bali kwa ajili ya kuwajibika kwa pamoja na kuimarisha utendaji wa serikali." **WR14**

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

Kauli hii inajenga uaminifu, kwani inajikita katika matumizi ya hoja zenye mantiki na ushawishi. Mnenaji alionyesha mtazamo wa kina kuhusu ushirikiano wa kisiasa kwa kusisitiza kwamba upinzani haupaswi kuchukuliwa kama chanzo cha migawanyiko, bali kama chombo cha kuimarisha uwajibikaji na utendaji wa serikali. Hii inaonyesha uelewa wa kina wa dhana ya demokrasia, ambapo nguvu ya upinzani si ya kupinga tu bali pia ya kushiriki katika uundaji wa sera bora kwa taifa. Kauli hiyo iliimarisha taswira yake kama kiongozi anayeheshimu mchango wa upinzani, jambo ambalo linawafanya wapiga kura kumwona kama kiongozi shirikishi badala ya mtawala wa kiimla. Kupitia hili, mnenaji anajenga mazingira mema ya kuchochea heshima kutoka kwa hadhira.

***Matumizi ya Historia na Utaalamu wa Mgombea***

Msemaji anajionyesha kama mtu mwenye tajriba na historia katika uongozi wa nchi ya Kenya anaposema:

"Jaribio langu la kwanza la kutafuta uteuzi wa chama ili kugombea urais lilikuwa mwaka wa 2007... Jaribio langu la pili la uteuzi wa urais lilikuwa mwaka wa 2013... Leo najua bila shaka yoyote kwamba wakati umefika wa kuwakilisha "*hustlers*" ... Mimi ndiye Naibu Rais wa kwanza aliyechaguliwa na anayeendelea kuhudumu nchini Kenya... Na nitabaki milele na shukrani tele kwa rafiki yangu, Rais Uhuru Kenyatta, kwa ushirikiano wa mafanikio katika chaguzi tatu."

Katika kauli ya mgombea huyu, anajisawiri kama aliye na tajriba katika masuala ya kisiasa. Anadhihirisha hili kwa kutaja jaribio lake la kwanza la mwaka wa 2007 na la pili la 2013 la kuwania urais. Kwa sababu ya tajriba hii, inampa ujasiri wa kujiona bora na mtaalam wa kuwakilisha wanyonge "*hustlers*" katika uwaniaji wa mwaka wa 2022. Kwa kutathmini uzoefu huu, ana historia ya miaka kumi na mitano ya kushikilia ndoto yake ya kuwa kiongozi wa taifa. Miaka hii kumi na mitano (15), inamjengea historia yake ya uongozi na kujiwasilisha kwa hadhira kama kiongozi anayestahili kutetea mahitaji hasa ya *hustlers*. Isitoshe, mgombea huyu anaweka wazi kuwa tajriba na historia yake ya uongozi ilianza alipokuwa mwanafunzi katika chuo kikuu. Anasema kuwa uzoefu huu ulimsaidia katika kujenga msingi wa historia yake ya kisiasa. Anathibitisha hili kwa kusema:

Nimekuwa nikijihusisha na shughuli zinazohusiana na uongozi wa kisiasa tangu nilipokuwa mwanafunzi wa chuo kikuu. Bila shaka, sikuwa na fursa ya kuwania uteuzi wa urais, lakini nilianza kutoka chini kabisa katika ngazi ya chama. Nilijitahidi kupanda juu hadi nikawa kiongozi wa chama na hatimaye nikawa mbunge wa bunge la kitaifa nikiwa na umri wa miaka 31. Nilikuwa naibu waziri nikiwa na miaka 33, waziri wa baraza la mawaziri nikiwa na miaka 36, na mbunge wa upinzani nikiwa na miaka 37.

Kwa kusema alijihusisha na shughuli za kisiasa tangu akiwa mwanafunzi wa chuo kikuu, alilenga kuonyesha kuwa haikuwa mara yake ya kwanza. Alionyesha kuwa ana historia ndefu na uzoefu wa uongozi tangu alipokuwa mwanafunzi. Isitoshe, anataja nyadhifa mbalimbali alizoshikilia katika uongozi wake kama vile; naibu wa waziri, waziri wa baraza la mawaziri na mbunge wa upinzani. Kupitia nyadhifa hizi, utaalamu wake ulitajirishwa na hivyo, kuendeleza historia yake ya uongozi.

***Kujenga Dhana ya Uadilifu na Uaminifu***

Dhana hii ilijitokeza katika mfano ufuatao.

"Utawala bora ni ule unaowahusisha wananchi katika kila hatua ya maamuzi, kutoka kwenye kupanga hadi utekelezaji wa sera." **RO11**

Mnenaji anajiwasilisha kama kiongozi anayejali mahitaji ya wananchi kwa kusisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya serikali na wananchi. Utawala unaoendeshwa kwa misingi hii hujenga imani kati ya serikali na wananchi, hali inayosaidia kukuza mshikamano wa kijamii na uendelevu wa sera. Kauli yake kuhusu mifumo ya maoni ya wananchi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

inaonyesha kuwa anathamini maoni yao, hivyo kujenga taswira ya uadilifu na uaminifu. Viongozi wa kisiasa mara nyingi hutumia lugha yenye matumaini na maono ya baadaye ili kuwavutia na kuwahamasisha wapiga kura kuunga mkono maoni yao.

Odinga pia alihimiza uwekezaji katika sekta za kiuchumi zinazoweza kuzalisha ajira kwa vijana na kusaidia maskini kujikwamua kiuchumi. Alisema:

"Ajira sio tu haki ya kila Mkenya, bali ni daraja la kuwatoa watu kutoka kwenye umaskini hadi maisha bora" Nitahakikisha kuwa kuna usimamizi madhubuti wa fedha za umma kwa kufuatilia matumizi na kuhakikisha kuwa hakuna ufujaji wa rasilimali. **RO13**

Kwa kutoa ahadi hii**,** alijijenga kama kiongozi mwadilifu na mwaminifu kwa kuhakikisha kuwa rasilimali zingetumika kwa manufaa ya wananchi. Alionyesha kuwa alipinga ufisadi na alikuwa na nia ya kuweka nidhamu katika matumizi ya mali ya umma. Kwa kusisitiza matumizi sahihi ya rasilimali, alijijengea taswira ya kiongozi anayeheshimu uwazi na anayepinga matumizi mabaya ya mali ya umma. Hii inaonyesha kwamba alikuwa na nia ya kujenga utawala bora unaozingatia uwajibikaji na matumizi mazuri ya rasilimali za taifa.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulionyesha kuwa wagombea wa urais, walitumia kwa ustadi aina tatu kuu za balagha. Matumizi ya kigusahisi yalijitokeza kwa kiwango cha juu zaidi ikilinganishwa na aina zingine za balagha. Hivyo, balagha ni muhimu sana katika ushawishi wa hadhira lengwa. Walio na ujuzi wake, huweza kufanikiwa zaidi katika kuwasilisha mawazo yao katika mawasiliano. Wagombea wote walidhihirisha ujuzi wa matumizi ya balagha hivyo kufanikiwa katika jumbe zao.

Wagombea wa kisiasa wanapaswa kutumia balagha kwa njia inayowajibika, yenye maadili, na inayolenga kushawishi kwa hoja za mantiki badala ya udanganyifu au kughilibu hisia za wapiga kura. Mashirika ya uraia yanapaswa kutilia mkazo uhamasishaji wa wapiga kura kuhusu umuhimu wa kuchanganua hotuba za kisiasa kwa msingi wa mantiki na maadili badala ya kushawishiwa na hisia pekee. Vyuo vikuu vina jukumu la kuimarisha elimu ya balagha kwa kuijumuisha katika mitaala ya isimu na mawasiliano. Hii itawapa wanafunzi ujuzi wa kuchanganua na kuelewa mikakati ya ushawishi inayotumika katika mawasiliano. Tafiti zijazo zifanye ulinganishaji wa mikakati ya balagha inayotumika na wahusika mbalimbali wa kisiasa katika miktadha tofauti ya kisiasa na kitamaduni.

## MAREJELEO

Al-Aadili, N. M. (2024). A Pragmatic Study of Derogation in American Election Campaign Speeches. *Theory & Practice in Language Studies (TPLS)*, *14*(3). 756–62. https://doi.org/10.17507/tpls.1403.16.

Aristotle. (1954). *The rhetoric of Aristotle* (W. Rhys Roberts, Trans.). Modern Library. (Original work written ca. 330 BCE)

Benoit, K., & Laver, M. (2003). Estimating Irish party policy positions using computer wordscoring: The 2002 election–a research note. *Irish political studies*, *18*(1), 97-107.

Gerstlé, J., & Nai, A. (2019). Negativity, emotionality and populist rhetoric in election campaigns worldwide, and their effects on media attention and electoral success*. *European Journal of Communication*, *34*(4), 410–444. https://doi.org/10.1177/0267323119861875

Grimaldi, W. M. A. (2020). Studies in the philosophy of Aristotle’s rhetoric. In R. L. Enos & L. P. Agnew (Eds.), *Landmark essays on Aristotelian rhetoric* (Vol. 14, pp. 15–159). Routledge.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Habwe, J. H. (2016). *Discourse analysis of Swahili political speeches* [Doctoral dissertation, University of Nairobi]. HAL Open Science. https://shs.hal.science/tel-01257830v1

Haucsa, G. M., Marzuki, A. G., Alek, A., & Hidayat, D. N. (2020). Illocutionary speech acts analysis in Tom Cruise's interview. *Academic Journal Perspective: Education, Language, and Literature*, *8*(1), 11-19.

Higgins, C., & Walker, R. (2012, September). Ethos, logos, pathos: Strategies of persuasion in social/environmental reports. In *Accounting forum* (Vol. 36, No. 3, pp. 194-208). https://doi.org/10.1016/j.accfor.2012.02.003.

Kamuhabwa, L. R. (2021). Aristotle on rhetoric and political persuasive skills: examples from political campaigns in African politics. *International Journal of Humanities, Philosophy And Language (IJHPL)*. 78–95. https://doi.org/10.35631/IJHPL.413006.

Karanja, J. M. (2022). 'Hustlers versus Dynasties': contemporary political rhetoric in Kenya. *SN Social Sciences*, *2*(10), 1–17. https://doi.org/10.1007/s43545-022-00541-2

Madon, H., Fadzil, I. L. M., & Rahmat, N. H. (2021). A rhetorical analysis of news article on work from home. *European Journal of Applied Linguistics Studies*, *3*(2). 22–36. https://doi.org/10.46827/ejals.v3i2.239.

Nurkhamidah, N., Fahira, R. Z., & Ningtyas, A. R. (2021). Rhetorical analysis of Joe Biden's inauguration address. *JL3T (Journal of Linguistics, Literature and Language Teaching)*, *7*(2), 73-82. 73–82. https://doi.org/10.32505/jl3t.v7i2.3371.

Nyako, I. D. (2013). *Language, Power, and Ideology: A Critical Discourse Analysis of Selected Speeches of Nana Addo Dankwa Akufo-Addo and John Dramani Mahama* (Doctoral dissertation, University of Ghana).

Qotrunnada, L. M. (2020). *Rhetorical style analysis of Hillary Clinton's speech*. Uin Sunan Ampel Surabaya.

Siti, M.K & Nyun,CT.,(2022). Logos, pathos and ethos in Mahathir Mohamad's speeches during his comeback as prime minister of Malaysia. *Trends in Undergraduate Research*, *5*(1), f1-15. https://doi.org/10.33736/tur.4539.2022

Torto, R. T. (2020). Aristotelian rhetorical theory as a framework for analyzing advertising texts in the print media in Ghana. https://doi.org/10.17507/tpls.1003.02.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.